Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**BAHATI MTEGA NA FLOWIN MTWEVE**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHAURI Na. 009/2019**

**HUKUMU KUHUSU USTAHIKI NA FIDIA**

**26 JUNI 2025**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 26 Juni 2025**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa hukumu katika kesi ya *Bahati Mtega na Flowin Mtweve dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Bahati Mtega na Flowin Mtweve (hapa wanarejelewa kama "Waleta Shauri wa Kwanza na wa Pili" mtawalia na kama "Waleta Shauri" kwa pamoja) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ("Mjibu Shauri"). Wakati wa kuwasilisha Shauri hili, walikuwa wamefungwa katika Gereza la Ruanda jijini Mbeya, wakitumikia kifungo cha maisha na viboko 12 vya kufuatia kusikilizwa kesi yao, kukutwa na hatia, na kuhukumiwa kwa ubakaji wa kikundi. Waleta Shauri walidai kufanyiwa ukiukaji wa haki zao wakati wa kusikiliza kesi dhidi yao katika mahakama za ndani.

Mjibu Shauri alipinga mamlaka ya Mahakama pamoja na ukubalifu wa Shauri hili.

Kuhusiana na mamlaka ya Mahakama, Mjibu Shauri hakutoa maelezo yoyote kuhusu madai ya kukosa mamlaka. Hata hivyo, kwa kuzingatia maagizo ya Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Mahakama ("Kanuni"), Mahakama iliendelea kutathmini vipengele vyote vya mamlaka yake ya kisheria. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kwamba, kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa unahusu haki zilizohakikishwa chini ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ambao Mjibu Shauri ni Mhusika, ilikuwa na mamlaka ya kisheria ya kushughulikia Shauri hili.

Mahakama pia ilibaini kwamba ilikuwa na mamlaka binafsi kutokana na kwamba, Mjibu Shauri alikuwa Mhusika wa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Itifaki") na alikuwa ameweka Azimio linalohitajika chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, likimruhusu Mleta Shauri kuwasilisha Shauri. Ingawa Mjibu Shauri aliondoa Azimio lake mnamo tarehe 21 Novemba 2019, Mahakama imeamua hapo awali kwamba uondoaji huo haukuwa na athari ya kurudi nyuma na haukuathiri Mashauri yaliyowasilishwa kabla ya kuondoa Azimio lake, kama shauri hili.

Mahakama pia ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya muda, kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea baada ya Mjibu Shauri kuwa Mhusika wa Itifaki, tarehe 10 Februari 2006. Mwisho, Mahakama ilihitimisha kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, kwani ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulifanyika ndani ya eneo la Mleta Shauri.

Mahakama ilibaini kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, inahitajika kutathmini ukubalifu wa kesi zote mbele yake. Katika kesi hii, Mjibu Shauri alipinga ukubalifu wa Shauri hili kwa sababu kwamba taratibu za ndani hazikukamilika.

Kuhusu pingamizi la Mjibu Shauri kwa madai kwamba Waleta Shauri walishindwa kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibaini kwamba takwa hili lilikuwa limetimizwa. Waleta Shauri walikuwa wamefuata taratibu zote zilizopo za mahakama, wakikata rufaa kwanza kwenye Mahakama Kuu na hatimaye kwenye mahakama ya juu ndani ya mfumo wa kisheria wa Mjibu Shauri, yaani, Mahakama ya Rufaa. Mahakama pia ilibaini kwamba Shauri hili liliwasilishwa tu baada ya Mahakama ya Rufaa kutoa hukumu yake. Mahakama iliendelea kuona kwamba kutaka kufanya mapitio ya uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ni suluhu isiyo ya kawaida ambayo Waleta Shauri hawakulazimika kuikamilisha. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi hili la Mjibu Shauri.

Mahakama ilibaini kwamba hakuna pingamizi lililotolewa kuhusu matakwa ya ukubalifu chini ya Kanuni ya 50(2)(a), (b), (c), (d), (f), na (g) ya Kanuni za Mahakama ("Kanuni"). Hata hivyo, iliendelea kutathmini matakwa haya ili kuhakikisha kwamba Shauri hili linakidhi viwango vyote vya ukubalifu vinavyohitajika.

Kwa hivyo, Mahakama ilibainisha kuwa Waleta Shauri walikuwa wametambuliwa kwa udhahiri kwa majina yao katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a). Iliona pia kwamba madai ya Waleta Shauri yalilenga kulinda haki zao kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Shauri hili lilitimiza Kanuni ya 50(2)(b) za Kanuni

Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Shauri husika haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Shauri au taasisi zake, kwa hivyo, Shauri lilitimiza Kanuni ya 50(2)(c) za Kanuni. Shauri hili pia halikutoka tu na habari zinazosambazwa kupitia vyombo vya habari kwani lilitokana na nyaraka za mahakama kutoka mahakama za ndani za Mjibu Shauri katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) za Kanuni.

Kuhusiana na sharti la kwamba Shauri liwasilishwe ndani ya wakati unaofaa, Mahakama ilirejelea kwamba si Mkataba wala Kanuni zilizotaja muda kamili ambao Shauri lazima liwasilishwe baada ya taratibu zote za ndani kukamilika. Badala yake, ufaafu wa muda huo unatathminiwa kwa msingi wa kesi kwa kesi. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kwamba Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wake tarehe 3 Agosti 2016, na Shauri hili liliwasilishwa tarehe 22 Machi 2019, ambacho ni kipindi cha miaka miwili, miezi saba, na siku kumi na tisa. Baada ya kutathmini muda kwa kuzingatia busara yake ya kisheria, na kwa kuzingatia hali ya Waleta Shauri kuwa watu wasiojua sheria, waliokuwa wamefungwa na ambao hawakuwa na uwakilishi wa kisheria wakati wa kusikiliza kesi za ndani, Mahakama ilibainisha kuwa kipindi cha miaka miwili, miezi saba na siku kumi na tisa kilikuwa kipindi kinachofaa kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama.

Mwisho, Mahakama ilibaini kwamba suala hilo halikuwa limesuluhishwa hapo awali na utaratibu mwingine wa kimataifa, na hivyo kutimiza matakwa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(g) za Kanuni. Kwa hivyo, Mahakama iliamua kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kisha Mahakama iliangalia endapo Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 2, 3, 5, na 7 vya Mkataba.

Mahakama ilisisitiza kwamba mzigo wa uthibitisho wa madai ya ukiukaji wa haki ya kutobaguliwa uko kwa upande wa mshtaki, ambaye lazima awasilishe ushahidi unaoonyesha ubaguzi kinyume cha sheria miongoni mwa watu walio katika hali kama yake. Katika Shauri hili, Mahakama ilibaini kwamba Waleta Shauri walishindwa kutoa ushahidi wowote ili kuthibitisha madai yao kuhusu ubaguzi. Kwa hivyo, Mahakama iliamua kwamba madai ya ukiukaji wa Kifungu cha 2 hayana mashiko na hivyo kutupilia mbali madai hayo.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki yao ya usawa na ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilibaini kwamba Waleta Shauri walikuwa wametoa madai ya jumla kuhusu ukiukaji wa haki zao. Hawakutoa hoja mahususi wala kuwasilisha ushahidi wowote wa kuunga mkono madai yao. Kwa sababu ya kukosekana kwa uthibitisho, Mahakama iliona kwamba Waleta Shauri walishindwa kuthibitisha ukiukaji wa Kifungu cha 3 cha Mkataba na kwa hivyo ilitupilia mbali madai hayo.

Waleta Shauri pia walidai kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki yao ya utu kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika kwa kuwahukumu adhabu ya kuchapwa viboko. Walidai kuwa hukumu ya kuchapwa viboko 12 ilisababisha madhara ya kimwili na kihisia, ambayo, kwa maoni yao, ulikuwa ukiukaji wa wazi wa marufuku ya Mkataba dhidi ya vitendo vya kikatili, vya kinyama, au vya kudhalilisha.

Ikirejelea busara yake ya awali ya kisheria, Mahakama ilithibitisha kwamba adhabu ya viboko ipo kinyume na Kifungu cha 5 cha Mkataba. Ilibainisha kkwamba msimamo huu unaendana na matokeo ya Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika kesi hii, wakati rekodi haikuonyesha endapo adhabu hiyo ilitekelezwa au la, Mahakama ilibaini kuwa kuwepo kwa sheria inayoruhusu adhabu ya viboko na Mahakama ya Mjibu Shauri kutoa adhabu ya viboko kulikiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Waleta Shauri walidai tena kwamba Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 7 cha Mkataba kwa kushindwa kuwapa uwakilishi wa kisheria wakati wa kusikiliza kesi za ndani. Walisema kwamba kitendo hiki kiliwanyima haki yao ya kusikilizwa kwa haki kama ilivyohakikishwa chini ya Mkataba.

Mahakama ilibaini kuwa Waleta Shauri hawakuwakilishwa na wakili katika hatua yoyote ya kusikiliza kesi za ndani. Hata hivyo, walikiwa wameshtakiwa kwa kosa kubwa la ubakaji wa kundi, ambalo lilikuwa na hukumu ya lazima ya kifungo cha maisha. Mahakama iliona kwamba, katika mazingira hayo, masilahi ya haki yalihitaji utoaji wa msaada wa kisheria bila malipo, bila kujali endapo Waleta Shauri walikuwa wameomba. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba wa Afrika, kikisomwa pamoja na Kifungu cha 14(3)(d) cha ICCPR, kwa kushindwa kuwapa Waleta Shauri uwakilishi wa kisheria wakati wa kusikiliza kesi za ndani.

Baada ya kubaini kwamba Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 5 na cha 7(1)(c) cha Mkataba, Mahakama iliona kwamba ukiukaji wa haki za Waleta Shauri za utu na za kusikilizwa kwa haki ulihalalisha kupewa fidia ya hasara ya kimaadili. Ingawa Waleta Shauri waliomba fidia ya TZS 100,000,000 kila mmoja, Mahakama iliona kwamba kiasi hicho ni kikubwa zaidi, kwa kutumia kanuni ya usawa, ilitoa TZS 300,000 kwa kila Mleta Shauri kama fidia ya haki kwa hasara ya kimaadili. Hata hivyo, Mahakama haikutoa fidia kwa sababu Waleta Shauri hawakubainisha wala kuthibitisha madhara yoyote ya kimwili yaliyotokana na ukiukaji huo.

Mahakama pia ilifuta hukumu ya kuchapwa viboko 12. Hata hivyo, Mahakama haikuona sababu za kulazimisha Waleta Shauri waachiliwe huru. Kwa hivyo, ombi la kuachiliwa huru lilitupiliwa mbali.

Mahakama pia iliamuru Mjibu Shauri afute vifungu vinavyohusu adhabu ya viboko katika sheria zake za uhalifu ili kutii Kifungu cha 5 cha Mkataba ndani ya mwaka mmoja baada ya taarifa ya uamuzi wa Mahakama kutolewa.

Madai ya Mleta Shauri wa Kwanza ya kurejesha afya yake kulingana na hali yake ya VVU yalitupiliwa mbali kwa kukosa uthibitisho na kushindwa kuonyesha uhusiano kati ya hali yake na ukiukaji uliobainishwa.

Kuhusu utekelezaji na utoaji ripoti, Mahakama iliamuru Mjibu Shauri, ndani ya miezi sita tangu tarehe ya taarifa ya hukumu hii kutolewa, awasilishe kwake ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na baada ya hapo, kila baada ya miezi sita hadi Mahakama itakapoona kuwa kumekuwa na utekelezaji kamili.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamuru kwamba kila mhusika abebe gharama zake.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0092019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*